**Kila mtu ana malaika (10) - Ujauzito na ukimwi katika ndoa**

Mwandishi: Romie Singh - Mhariri: Saumu Mwasimba

**Wahusika**

Angela
Pinto
Djamila
Annie
Nesi

**UTANGULIZI**

Karibu tena katika kipindi cha Sikiliza Ujifunze, ambapo leo tunaingia katika sehemu ya 10 na ya mwisho ya mchezo wa kuigiza "Malaika wa Kila mtu", mchezo unaofuatilia maisha ya vijana wanne kuhusu tabia zao katika masuala ya ngono na hatari za kimaisha wanazokumbana nazo.

Angela anataka kujifungua salama na kupanga maisha yake ya baadae na mpenzi wake Pinto pamoja na mtoto wao, lakini vipi watafanikiwa katika hilo ikiwa wote wana virusi vya HIV? Je, inawezekana? Tega sikio.

**SURA YA KWANZA: KWENYE BUSTANI**

| | |
|---|---|
| SFX | SAUTI ZA NDEGE;ASUBUHI |
| SFX | MKEBE WA BISKUTI UNAFUNGULIWA |
| ANGELA | Shika Djamila! Chukua biskuti nyingine! Lo shoga, stori yako utadhani ni sinema, enhe nieleze kisha nini kikatokea? |
| DJAMILA | Nilimng’ata nakwambia Angela. (Wacheka) Nikakimbia! |
| ANGELA | Eti nini? Hongera shoga ulifanya vizuri sana! |
| DJAMILA | Ilibidi swahiba, ningefanyaje, ningefanya mchezo angenibaka mshamba yule, alikuwa akinuka pombe. |
| ANGELA | Urgh! Unyama gani jamani! (Kimya kidogo) Nakuulizaje Djamila rafiki yangu, ulipomng’ata ulifyonza damu? |
| DJAMILA | Huh swali gani hilo? |
| ANGELA | Djamila nakuuliza tu, yeye alitokwa damu? |
| DJAMILA | Hapana, sikumng’ata sana. Kwa nini wauliza? |
| ANGELA | Aanha hapo sawa. Angekuwa katokwa damu hapo… |
| DJAMILA | Mungu wangu Angela, usiniambie mjomba anaweza kuwa ana ukimwi? |
| ANGELA | Anha, sio Ukimwi. Wajua Djamila, ukimwi ni hatua ya mwisho pale unapokuwa huna tena kinga ya mwili, lakini mtu ye yote anaweza kuishi na virusi vya HIV na akawa mnene mwenye afya zake. Na ndo sababu madaktari, wauguzi, na wengineo huvalia gloves za |

| | |
|---|---|
| | kuwakinga wasije wakajihatarisha kuambukizwa, maana unajua virusi vya HIV vinaambukiza kupitia damu. Hata kupitia mate! Na mtu akibakwa, inabidi apate matibabu ya kumzuia asiambukizwe virusi vya HIV katika muda wa saa 72. |
| DJAMILA | Lo, nashukuru hayakufika mbali. Lakini mamangu ataniua akisikia namshutumu mtu ye yote kwenye familia kwamba ameambukizwa virusi vya HIV. Oh, pole Angela, sikudhamiria ku… |
| ANGELA | Hakuna neno. Lakini unajua haipaswi kuwa shutuma Djamila. Ukweli ni kwamba katika sehemu zingine unajua zaidi ya mtu mmoja katika kila watu watano wameambukizwa. Inatubidi tuache kuwatuhumu watu na kuwalaumu na tuzungumze kwa uwazi. Sio wote wanaoambukizwa virusi ni kwa sababu ya kufanya kitu fulani. |
| DJAMILA | Ni kweli Angela, wasichana wanabakwa kila siku, mara nyingine ni kwa sababu wao ni mabikra. Unajua wanaume wana fikra potofu sana - wengine wanaamini kwamba wakilala na bikra, basi watapona. Na hapo wa kulaumiwa sio msichana. |
| ANGELA | Ndio, sio kosa la msichana kabisa. Au kwa mfano umeongezwa damu iliyo na virusi kwa bahati mbaya - watu wengine wanadhani wanaoambukizwa virusi ni wasichana wenye tabia chafu tu. Lakini nilikuwa bikra, na wewe pia pengine sio msichana mwenye tabia ya uzinzi. Lakini siku moja tu inaweza kukuponza ukaambukizwa HIV. |
| DJAMILA | Kweli Angela. Nafikiri wewe ni jasiri wa hali ya juu. Hebu angalia maskini ulikuwa hujui lolote, hukujua hata ujauzito nini, na sasa unakaribia kuitwa mama! Na isitoshe swahiba yangu, umekuwa mjuzi wa mambo mengi - umegeuka sana rafiki yangu na sasa umekuwa malaika wa kweli. |
| SFX | MUZIKI UNAFUNGA |

**SURA YA PILI: ASUBUHI NA MAPEMA**

| | |
|---|---|
| SFX | JIKONI; SAUTI ZA VYOMBO VIKIOSHWA; PINTO ANAKOHOA |
| ANGELA | (Kando ya Mic) Pinto, tarehe ya kwenda kujifungua ni 25. |
| PINTO | (Asafisha meza) kwa hiyo ni wiki mbili kutoka sasa! Halafu utatoka lini hospitali? |

| | |
|---|---|
| ANGELA | (Kando ya Mic) kila kitu kikienda sawasawa, nafikiri ntatoka baada ya siku chache tu. |
| PINTO | Basi hakuna neno, kila kitu kiko tayari hapa kwa ajili ya mwanetu! Tumelo wajua ni mtoto wa kiume, kwa hiyo jina la kinyumbani kabisa ndo linalofaaa. Na jina hilo linamaanisha imani… sasa mpenzi wangu Angela, wataka kitambaa hiki cha mezani nikiweke wapi? (Akikohoa) |
| ANGELA | (Kando ya mic) Kitumbukize tu kwenye droo la kabati pale. (Kwenye mic) Ah, nisije nikasahau dawa zangu. |
| SFX | SAUTI YA KUNYWA MAJI KWA PUPA |
| ANGELA | Phew! Aah, acha nikae. (Apumua) Pinto. Umeshawahi kufikiria nini kitatutokea katika miaka michache ijayo? |
| PINTO | Tafadhali bwana mazungumzo gani hayo, sijafikiria na wala sitaki kufikiria huko. |
| ANGELA | Tunaishi na virusi vya HIV Pinto, tunaweza kuwa wagonjwa na tukashindwa kumlea mtoto wetu (taratibu) twahitaji kuwa na familia, lakini mamangu hajui hali yetu, wala mjomba wangu Billy. |
| PINTO | Sasa wapendekeza nini? Wataka tukawaambie tuna virusi vya HIV? Mungu wangu ndo watatukasirikia hawatatuzungumzisha tena. (Akohoa) |
| ANGELA | Itatubidi tuwaambie ili wajiandae. Mtoto wetu anahitaji kuwa na mtu wa kumlea ikiwa cho chote kitatokea kwetu. |
| PINTO | (Akilia) Angela siwezi, siwezi kufanya hivyo. Nataka lakini sina ubavu. |
| ANGELA | (Kwa unyonge) Kuna kundi la kutoa usaidizi linajiita Ishi na matumaini. |
| PINTO | Ah Angela bwana usiniambie ni kundi la watu kutoa hadithi zao na kuambizana juu ya vipi mtu kafikia kupata virusi hivyo, na bla bla, tafadhali Angela. |
| ANGELA | Hapana Pinto, kundi hilo haliko hivyo unavyofikiria. |
| PINTO | Wewe umejuaje? |
| ANGELA | Nilikutana nao kliniki, kuna waume na wake zao - wengine mke ana virusi mume hana, ndo hali ilivyo wengine wote wawili wana virusi kama sisi. |
| PINTO | Sasa wanazungumza kuhusu nini? |
| ANGELA | Wanazungumza kila kitu, mambo yote, wanacheka. Pengine Pinto tujiunge nao siku moja ujionee. Kwa kweli Pinto tunahitaji msaada kutoka kwa watu ambao wana watoto na ambao tayari wanajua nini wanatarajia, tuwashirikiane na wenzetu wanaoishi na virusi vya HIV kama sisi. |

PINTO Najua, naelewa.

ANGELA (Kwa upole) Pinto, lazima uikubali hali yako. Tunaweza hata kuishi kwa muda mrefu tukaepuka kufikia kiwango cha kuwa na maradhi kamili ya ukimwi, ikiwa tutakuwa na uwazi na kuaminiana. Tafadhali Pinto, tuchukue hatua kabla maji hayajamwagika. Nenda kapime kwa ajili ya mwanao tu. Maisha yako yatabadilika.

SFX MUZIKI WA KUFUNGA

**SURA YA PILI: KWENYE OFISI YA KLINIKI**

NESI Sasa Angela, tunajua kiwango chako cha kinga ya mwili, lakini ya Pinto hatuijui mpaka aje apimwe. Hatuwezi kukisia tukasema iko kama yako.

ANGELA Hata yule bwana katika kundi lile la kuwasaidia wenye virusi kanambia hivyo hivyo. Lakini nadhani Pinto atakubali kuja pima. Alitiwa moyo sana na jinsi alivyowaona wenzake wanaoishi na HIV walivyo na furaha na kuishi kama kawaida. Na vile walivyokuwa wanazungumzia hali zao kwa uwazi.

NESI Ni jambo zuri kumtia moyo, lakini usimlazimishe. Ni lazima akubaliwe kwa hiari bila ya kushurutishwa na mtu, apate ushauri nasaha, apimwe, halafu ashauriwe tena baada ya kupimwa. Ikiwa matokeo ya uchunguzi yataonyesha inabidi aanzishiwe matibabu ya kutumia dawa za kupunguza makali ya HIV, basi mtaweza kutiana moyo. Mpike pamoja na kila siku wenyewe mjinafasi… na

NESI NA ANGELA KWA PAMOJA: Tujamiiane kwa kutumia Kinga. (Wacheka)

**SURA YA TATU: NDANI**

SFX WATAYARISHA CHAI. SAUTI YA VIKOMBE

ANGELA Angalia hata sio safari ndefu kuja kuniona!

DJAMILA Hapana! Zaidi kidogo ya dakika 45. Lo umenenepa swahiba.

ANGELA Nakwambia Pinto anataka kumuita Drogba maanake sivyo anavyorusha mateke.

ANNIE (Kando ya Mic) Karibuni chai, iko tayari. (Kwenye mic) Jiko lako zuri shoga.

DJAMILA Wow, kweli linapendeza, nyumba nzima kwa ujumla ni kiboko, nakubaliana na wewe Annie.

ANGELA Asanteni (akikoroga chai) enhe, nipasheni kipi kipya Annie? Djamila.

DJAMILA Basi mwenzenu nimepiga ile nambari ya simu ya watu wanaotoa maelezo juu ya ukimwi kwa njia ya simu!

ANGELA Wacha maskhara! Kwa nini ulipiga?

DJAMILA Wajua, nilikuwa na wasiwasi sana kwamba mamangu huenda akamtetea nduguye dhidi yangu nikimwambia jinsi alivyojaribu kuniparamia. Kwa hiyo nikaona bora niulize ushauri kwa hao washauri kwa njia ya simu.

ANGELA Halafu ikawaje?

DJAMILA Huyo mwanamke nilozungumza nae akapendekeza nipige simu kwa washauri wenzao lakini wa dini ya kiislamu, mimi mwenyewe nilishangaa kumbe kuna huduma kama hiyo.

ANNIE Ni jambo la kutia moyo sana, kwa kweli ni jambo zuri, sote tunataka kujua wapi pahala pa salama tukimbilie kupeleka matatizo yetu, bila ya kujali kabila, rangi, au dini tunayotoka. Kuna mambo chungu nzima kila mahali tunaambiwa ni mwiko kuyafanya. Inatisha kwa kweli.

ANGELA Nakubaliana na wewe. Na mjomba wako Imrat?

DJAMILA (Akinywa chai) Lo, ni kama katoweka kabisa!

ANNIE Katoweka bila ya kiganja chake cha mkono wa kulia…!

WOTE WANACHEKA

ANNIE Mie pia baba sukari wangu Jet kaingia mitini.

DJAMILA Nakwambia ametulia tangu aachane na huyo mzee.

ANNIE (Acheka) Djamila ana raha kwa sababu sasa tuko pamoja katika mradi wa shule wa somo la sayansi. Na wamkumbuka Spike yule alokuwa mpenzi wangu, dereva wa texi? Alikamatwa kwa kuiba simu, kwa hiyo nashukuru kila kitu kwangu waaaaa. Sasa naishi maisha yangu.

DJAMILA Na Tom! Nakwambia huwezi kuamini! Anatusaidia sana katika mradi wetu na tena yuko hapa na hapa na Annie mimi ndo niko katikati yao!

ANGELA Lo, mwanishangaza. Lakini Tom siku zote alikuwa akikutaka Annie. Lakini wewe?

ANNIE Ni marafiki tu wa kawaida, hakuna cha ziada. Hatufanyi cho chote! Naona raha sana.

ANGELA Wataalamu wanasema inafaa mukae wiki sita bila ya kuonana kimwili kabla ya kupimwa. Wanakiita kipindi cha kusubiri.

ANNIE (Kwa sauti ya uchungu) Sawa, nitafanya hivyo, naahidi.

DJAMILA Na TV ya Ma Tilly imevunjika, kwa hiyo hakuna teeena kuangalia vipindi vya michezo ya kuigiza!

| | |
|---|---|
| ANNIE | Ndio imevunjika, lakini tuna afadhali sasa kimaisha kwa sababu mama amepata kibarua cha siku. Angalau anaweza kusimamia karo yangu ya shule, hiyo si nafuu! Na pia ananipikia. |
| ANGELA | Tutafaulu mashoga! Tuishi salama katika ulimwengu huu wa HIV na ukimwi. Natumai Pinto wangu atakubalia kwenda kupimwa na kushauriwa kwa hiari hivi karibuni. Ndo tuweze kupanga maisha yetu na ya mtoto wetu Tumelo. |
| DJAMILA | Tumelo! Mtoto wetu mtamwita Imani! Jina safi. |
| ANNIE | Atakuwa malaika kama wewe! |
| ANGELA | Kama ninavyosema kila siku. |
| Kwa pamoja | "Kuna malaika kwa kila mtu" |
| ANGELA | (Akicheka) Mmejuaje ntasema hivyo? Njooni niwaonyeshe atakapolala mwanangu. Ni mkubwa sana. Namsikia akirusha viteke vyake. |

**Hitimisho**

Msikilizaji umesikia mambo yalivyokuwa katika mchezo wa kuigiza "Malaika wa kila mtu" ambapo leo ilikuwa ni sehemu ya mwisho ya mchezo huo. Wahusika wakuu katika mchezo huo walikuwa ni

ANGELA………
DJAMILA………
ANNIE ………..
JET …………….
TOM…………..
PINTO…………

Wengine walioshiriki ni……………

Kipindi cha sikiliza ujifunze kutoka DW idhaa ya Kiswahili kimedhaminiwa na wizara ya mambo ya nje ya Ujerumani na kimeandaliwa katika lugha sita. Kumbuka ukitaka kusikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine, nenda kwenye tovuti yetu, anuani ni www.dw-world.de/lbe.

Mchezo wa kuigiza wa malaika wa kila mtu umeandikwa na Romie Singh na kuhaririwa na Saumu Mwasimba.

Kwa herini.